

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu: "MAKAMU",
Simu Na.: +(255)026 2329006
Nukushi.: +(255)026 2329007/2983150
Barua Pepe: km@vpo.go.tz



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S. L. P. 2502,
40406 DODOMA,
TANZANIA.

22 Septemba 2026

TAARIFA KWA UMMA
MAKAMU WA RAIS KUHUTUBIA KIKAO CHA 81 CHA BARAZA KUU LA UMOJA
WA MATAIFA.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Deogratius Ndejembu leo Jumanne, Septemba 22, 2026, anatarajiwa kuhutubia Mjadala Mkuu wa Kikao cha 81 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 81), unaofanyika katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani.

Makamu wa Rais anamwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika mkutano huo wa ngazi ya juu unaowakutanisha Wakuu wa Nchi na Serikali, pamoja na wawakilishi wa ngazi za juu kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Mjadala Mkuu wa mwaka 2026 unafanyika chini ya kaulimbiu, "Kurejesha imani, kusimamia mabadiliko: Umoja wa Mataifa unaowatumikia wote" (Restoring trust, managing transformation: A United Nations that delivers for all).

Miongoni mwa mambo yanayojadiliwa katika mkutano huo ni changamoto mbalimbali zinazoikabili Dunia na namna ya kuimarisha ushirikiano katika kutafuta suluhisho la kudumu, hususan katika masuala ya amani na usalama wa kimataifa, maendeleo endelevu, mabadiliko ya tabianchi, afya, utawala wa teknolojia na Matumizi ya akili unde (AI), pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa.

Mjadala Mkuu wa Kikao cha 81 umeanza leo, Septemba 22, na utaendelea hadi Septemba 26, kabla ya kuhitimishwa Septemba 28, 2026.

Imetolewa na
Ofisi ya Makamu wa Rais
22 Septemba 2026
New York – Marekani.